

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِينَ كَانُوا يُنْكِرُونَ وَعَلَى الصَّابِرِينَ لِيَسْتَغْنُوُا هُنَّ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَغْنَفُ
الَّذِينَ مِنْ قَلْبِهِمْ وَلَيَسْكُنَنَّ لَهُمْ وَيَنْهَا اللّٰهُ أَنْقَعَنَّ لَهُمْ وَلَيَجِدُنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقِهِمْ أَنَّهُ
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاغِنُونَ



Na: 1445 H / 029

Jumanne, 9 Ramadhan 1445 H

19/03/2024 M

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

**Waislamu nchini China Wanalazimishwa Kufungua Saumu kwa Pombe na Dada zetu Nguo zao
Zinakatwa kuwa Fupi!**

(Imetafsiriwa)

Ajenda ya kilimwengu ya kukandamiza kitambulisho cha Kiislamu na kutumia unyanyasaji mkali kwa Ummah wa Muhammad (saw) iko hai na inatumika katika DOAMuslims, tovuti ambayo imebofea katika kunakili dhulma dhidi ya Waislamu, kupakia picha na kunukuu maeneo ambayo wanawake wa Kiislamu wanalazimishwa kukata nguo zao ziwe fupi. Haya ni matusi ya moja kwa moja na unyanyasaji wa kuwalilisha wanawake katika kudhihirisha kwao kujisitiri.

Pia kumekuwa na matukio mengi yaliyo nakiliwa ambapo Waislamu wanalazimishwa kufuturu kwa pombe. Vitendo hivi vya kuudhi vinaruhusiwa kutokea kwa vile kuna ufaamu unaojulikana vyema kuwa hakuna kizuizi katika kutusi matendo ya Kiislamu. Wanawake wachamungu wa Kiislamu wameachwa wakipuuzwa na kutelekezwa, kuaibishwa na kuumizwa mikononi mwa maadui wa Uislamu.

Kuna maelfu mengi ya Waislamu katika kambi za kufanyishwa kazi kwa lazima wakipangwa upya kisaikolojia ili kukumbatia maadili yasiyo ya Kiislamu katika mwezi huu wa Ramadhan. Watoto wa Waislamu nchini China mara nyingi huchukuliwa kutoka kwa wazazi wao na kupewa familia zisizo za Kiislamu. Hali hii ya kuudhi imekuwa katika mchakato mbele ya macho ya ulimwengu kwa miaka mingi.

Je, ni Ramadhan ngapi zaidi zitapita huku dada zetu wakilazimishwa kufunga uzazi na kukatazwa kuficha heshima zao hadharani?

Ni viongozi wangapi zaidi watakuja na kuondoka bila kufanya chochote kusaidia mateso na aibu yao? Yuko wapi kiongozi mchamungu, mkweli wa Waislamu wa kuukomboa Ummah kutoka kwa dhalimu wa Shirki!!??

Ni lazima tusimame dhidi ya mifumo inayoruhusu hili kutokea na kufanya kazi kwa kila juhudili ili kusimamisha Khilafah kwani ndio hitaji la dharura zaidi la wakati wetu. Watoto wetu hawawezi kugejeshwa na burudani zisizo na maana za dunia na lazima wakumbushwe wajibu wao wa kufanya kazi kwa namna ya Mtume (saw).

Imarisheni dua kwa dada zetu katika kipindi chao cha mitihani na hatutasahau wajibu wetu wa kufichua ukandamizwaji wao.

[وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِعِصْمٍ أُولَئِنَاءِ بَنْضٌ إِلَّا تَعْلُوَهُ تَنْنٌ فِتْنَةٌ فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ]

“Na wale walio kufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipo fanya hivi itakuwako fitna katika nchi na fisadi kubwa.” [8:73]

Kitengo cha Wanawake

katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

